GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXVII Nam. 6710 **27 Juni, 2018** **Bei Shs. 5,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na Kuweka Masharti ya Ukaguzi wa Elimu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo 145

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Mswada

Nam. : Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ya 2018

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 9 Mei, 2018 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR (Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
10 April, 2018 ***Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi***.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA
WA
SHERIA YA KUANZISHA OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU NA KUWEKA MASHARTI YA UKAGUZI WA ELIMU PAMOJA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ya 2018 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Matumizi.

2. Sheria hii itatumika kwa:

(a) Skuli zote zinazotoa elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari;

(b) Taasisi yoyote inayotoa mafunzo ya ualimu;

(c) Vituo vya Elimu Mbadala na Elimu ya watu wazima; na

(d) Taasisi za elimu zilizosajiliwa zilizo nje ya mfumo rasmi wa elimu.

Ufafanuzi.

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maudhui yatahitaji vyenginevyo:

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Ushauri iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria hii;

"Mkaguzi Mkuu" maana yake ni Mkaguzi Mkuu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 13 cha Sheria hii;

"Naibu Mkaguzi Mkuu" maana yake ni Naibu Mkaguzi Mkuu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 16 cha Sheria hii;

"Waraka" inahusisha pamoja na nyaraka nyenginezo ikiwemo: azimio la kazi, andalio la somo, kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi, kumbukumbu za kazi za kila siku za mwalimu na vifaa vingine vya skuli ambavyo Mkaguzi wa Elimu anaweza kuvihitaji kwa madhumuni ya Ukaguzi;

"Ukaguzi wa Elimu" maana yake ni utaratibu wa kufanya ziara za mara kwa mara katika skuli ili kuhakikisha kuwa zinafuata Sheria ya Elimu, Sera ya Elimu, Sheria hii na miongozo mingine ya Elimu ili kuimarisha utendaji katika skuli;

"Mkaguzi wa Elimu" maana yake ni Mkaguzi wa Elimu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 21 cha Sheria hii;

"Elimu rasmi" maana yake ni mfumo maalum wa elimu unaofuata mtaala rasmi unaotambulika;

"Mkuu wa Ukaguzi wa Mkoa" maana yake ni kiongozi wa Ukaguzi katika ngazi ya Mkoa aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria hii;

"Mfumo wa ukaguzi" maana yake ni miongozo ya uendeshaji wa ukaguzi wa Elimu Zanzibar;

"Msimamizi" maana yake ni mtu yeyote anaehusika na usimamizi na uendeshaji wa skuli;

"Waziri" maana yake ni Waziri anaehusika na Elimu;

"Wizara" maana yake ni Wizara inayohusika na Elimu;

"Ofisi" maana yake ni Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Skuli ya Binafsi" maana yake ni Skuli ambayo inamilikiwa na kuendeshwa kikamilifu na mtu au kikundi cha watu kisichokuwa Serikali ;

"Skuli" maana yake ni skuli zote zinazotoa elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari, au Taasisi yoyote inayotoa mafunzo ya ualimu, na vituo vya Elimu mbadala na Elimu ya Watu wazima, ambavyo vinatoa elimu rasmi na isiyo rasmi na vimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria;

"Viwango" maana yake ni daraja ya ubora uliofikiwa na skuli kwa kupima ufanisi wa viwango vya elimu na viashiria vyake kama vinavyoainishwa katika Mfumo wa Ukaguzi;

"Uthibiti Ubora" maana yake ni utaratibu wa upimaji na utoaji taarifa kuhusiana na Skuli katika kuhakikisha kuwa elimu bora inapatikana kwa mujibu wa viwango vya elimu vilivyowekwa kupitia utaratibu wa kufundisha na kujifunza;

"Ukaguzi wa ki Mkoa" maana yake ni Mfumo wa Ukaguzi wa Elimu ambao unafanyika katika Mkoa husika ndani ya Zanzibar.

SEHEMU YA PILI
UANZISHWAJI NA USIMAMIZI WA OFISI

Kuanzishwa kwa Ofisi.

4.-(1) Kunaanzishwa Wakala wa Serikali utakaojulikana kama Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na ufupisho wake utakuwa ni "OCIE"

(2) Ofisi, kwa kuthibitishwa na Waziri, itakuwa na uwezo wa:

(a) kupata, kuhodhi, kununua au kuhamisha mali inayohamishika na isiyohamishika;

(b) kuingia katika mkataba au muamala wowote kwa mujibu wa sheria;

(c) kufanya kitendo au kitu chochote ambacho kwa kawaida wakala zinazofanana nayo inaweza kupaswa kufanya kwa mujibu wa sheria;

Muhuri na Nembo ya Ofisi.

5.-(1) Kutakuwa na Muhuri na Nembo ya Ofisi yenye sura na ukubwa kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya Muhuri wa Ofisi katika waraka wowote yatathibitishwa kwa kuwepo kwa saini ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu au Afisa yeyote wa Ofisi aliyeidhinishwa na Mkaguzi Mkuu wa Elimu.

(3) Waraka utatambuliwa kuwa ni waraka sahihi uliotolewa na Ofisi iwapo waraka huo umetiwa muhuri wa Ofisi na kuthibitishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Malengo ya Ofisi.

6. Malengo ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ni:

(a) kuhakikisha kuwa elimu inatolewa kwa mujibu wa Sera, Sheria na miongozo ya Serikali;

(b) kuhakikisha taasisi zote zinafundisha kwa mujibu wa mitaala iliyoidhinishwa kwa ngazi husika;

(c) kuhakikisha kuwa miiko na maadili ya kazi ya ualimu inafuatwa;

(d) kushauri juu ya viwango bora vya ufundishaji na ujifunzaji, uongozi na uendeshaji, kuwasaidia wanafunzi na juu ya matokeo ya kujifunza; na

(e) kuhakikisha kuwa viwango vya elimu na uthibiti ubora vinafuatwa katika ngazi zote za skuli na kwenda sambamba na Miongozo ya Wizara.

Mfumo wa Ukaguzi wa Elimu.

7.-(1) Kutaanzishwa mfumo wa ukaguzi wa elimu utakaothibitishwa na Bodi ambao utakuwa ni muongozo mkuu wa ukaguzi utakao husisha mambo yafuatayo:

(a) Aina za ukaguzi na utaratibu wake ambazo ni:

(i) ukaguzi mkuu utakaofanywa kwa kila skuli kwa kuangalia viwango vya ufundishaji na ujifunzaji, uongozi na uendeshaji, msaada kwa wanafunzi na matokeo ya kujifunza;

(ii) ukaguzi wa ufuatiliaji utakaofanywa kwa kufuatilia utekelezwaji wa ushauri na mapendekezo yaliyotolewa katika ukaguzi uliopita;

(iii) ukaguzi wa masomo utakaofanywa kwa kumkagua mwalimu wa somo husika kwa kila skuli; na

(iv) ukaguzi wa kushtukiza utakaofanywa kwa ajili ya kutekeleza agizo kama itakavyoelekezwa na Katibu Mkuu wa Wizara.

(b) zana za ukaguzi na uandishi wa ripoti;

(c) maadili na miiko ya wakaguzi; na

(d) muongozo wa kufanyia ukaguzi wa ndani wa skuli kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa kwenye mfumo wenyewe wa ukaguzi

(2) Kila skuli kwa kawaida itakaguliwa mara moja kwa mwaka.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki ukaguzi wa skuli unaweza kufanyika kwa kadiri itakavyohitajika.

Uwasilishaji wa Ripoti za Ukaguzi.

8.-(1) Ripoti za ukaguzi zitawasilishwa kwa skuli na mamlaka husika kulingana na aina ya ukaguzi utakaofanyika ndani ya wiki mbili baada ya kufanyika ukaguzi.

(2) Ripoti ya ukaguzi wa skuli iliyokaguliwa, kwa Skuli za Sekondari itawasilishwa skuli na kwa Katibu Mkuu wa Wizara, na kwa upande wa Skuli za Maandalizi na Msingi ripoti husika zitawasilishwa skuli na kwa Mkurugenzi wa Manispaa, Baraza la mji au Halmashauri za Wilaya zinazohusika na skuli hizo.

(3) Ripoti za ukaguzi wa Taasisi na vituo vyengine vilivyoainishwa katika kifungu cha 2 (b), (c) na (d) cha Sheria hii zitawasilishwa kwa taasisi au kituo husika na kwa Katibu Mkuu wa Wizara.

Kazi za Ofisi.

9. Kazi za Ofisi zitakuwa ni:

(a) kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa skuli na mwalimu mmoja mmoja kama ilivyofafanuliwa katika Mfumo wa Ukaguzi uliowekwa na Ofisi;

(b) kuhakikisha kuwa mtaala uliokubalika ndio unaotumika kwa ajili ya kuleta ufanisi wa utowaji wa elimu katika skuli;

(c) kuweka viwango vya ukaguzi na viashiria vya utekelezaji ili kudumisha ubora wa skuli katika vipengele vya uongozi na uendeshaji, ufundishaji na ujifunzaji, msaada kwa wanafunzi na matokeo ya kujifunza;

(d) kufanya ukaguzi wa elimu kwa skuli inayopendekezwa kuanzishwa kabla ya kuanzishwa na kusajiliwa, na kutoa mapendekezo na ushauri kwa mamlaka zinazohusika kuhusiana na kusajili na kufuta usajili wa skuli, na kupandisha au kushusha vyeo kwa walimu na walimu wakuu;

(e) kusimamia utendaji wa walimu wakuu na walimu katika kutekeleza majukumu yao katika skuli kama yalivyoelekezwa katika Viwango vya Taaluma ya Ualimu na Maadili, Miongozo ya Wizara na Kanuni za Ukaguzi;

(f) kushajihisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa lengo la kuongeza ufanisi katika Ukaguzi wa Elimu;

(g) kuzielekeza skuli zilizokaguliwa juu ya mambo yanayohusu uimarishaji wa elimu bora kwa kuzingatia taarifa za utendaji wa skuli na ripoti za ukaguzi;

(h) kutoa ripoti ya kila mwaka ya ukaguzi wa elimu na kutoa mrejesho wa uthibiti ubora kwa wadau wa elimu;

(i) kufanya utafiti kwa kuzingatia mambo yaliyobainika katika ripoti za ukaguzi wa elimu; na

(j) kutekeleza kazi nyengine yoyote inayohusiana na ukaguzi kama itakavyoelekezwa na Waziri.

Kuanzishwa kwa Bodi ya Ushauri.

10.-(1) Kutakuwa na Bodi ya Ushauri ya Ofisi.

(2) Bodi ya ushauri itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkaguzi Mkuu wa Elimu;

(c) Mwakilishi kutoka Wizara inayohusika na Elimu;

(d) Mwakilishi kutoka Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa;

(e) Mwanamke mwenye utaalamu na uzoefu wa muda mrefu katika masuala ya ufundishaji;

(f) Mwakilishi mwenye utaalamu na uzoefu wa muda mrefu katika masuala ya elimu kutoka katika moja ya taasisi au chuo kikuu kinachotoa mafunzo ya ualimu ndani ya Zanzibar; na

(g) Mwakilishi mwenye utaalamu na uzoefu wa muda mrefu katika masuala ya Elimu kutoka katika moja ya taasisi au skuli binafsi ndani ya Zanzibar.

(3) Isipokuwa kwa wajumbe wanaoingia kwa nyadhifa zao, wajumbe wengine watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika.

(4) Utaratibu wa Bodi utakuwa kama unavyoelezwa katika Jadweli la Sheria hii.

Sifa za Mwenyekiti.

11. Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) mwenye angalau Shahada ya Kwanza katika fani ya elimu kutoka katika Chuo Kikuu kinachotambulika;

(c) mwenye uzoefu usiopungua angalau miaka kumi katika masuala ya Elimu; na

(d) mwenye kuheshimika katika jamii.

Kazi za Bodi ya Ushauri.

12. Kazi za Bodi ya Ushauri zitakuwa ni:

(a) kupitisha mpango kazi, bajeti na ratiba za Ofisi;

(b) kuwasilisha kwa Waziri ripoti ya mwaka ya ukaguzi na kumbukumbu za vikao vya Bodi mnamo mwezi wa tatu wa mwaka unaofuatia baada ya kukamilika kwa mwaka wa kalenda na kumpa taarifa kuhusiana na utendaji wa elimu Zanzibar na kushauri utekelezaji wake kama ilivyopendekezwa katika yaliyobainika katika ukaguzi;

(c) Kufanya mapitio ya taarifa za kila robo mwaka kuhusu uendeshaji wa Ofisi, ukaguzi wa hesabu na ukaguzi;

(d) Kupendekeza hatua za kinidhamu na kuwapandisha vyeo wafanyakazi wa Ofisi;

(e) Kupendekeza uteuzi wa Wakaguzi wa Elimu kwa Waziri;

(f) Kutoa mapendekezo kwa Waziri kuhusiana na kufungwa au kufunguliwa kwa skuli; na

(g) Kutoa ushauri kuhusu ubora wa elimu inayotolewa, ukaguzi wa elimu, taarifa za ukaguzi wa elimu na kupendekeza mikakati ya uimarishaji.

Uteuzi wa Mkaguzi Mkuu wa Elimu.

13.-(1) Kutakuwa na Mkaguzi Mkuu wa Elimu ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkaguzi Mkuu wa Elimu ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) mwenye angalau shahada ya uzamili katika fani ya elimu au inayolingana na hiyo kutoka katika Chuo Kikuu kinachotambulika;

(c) mwenye uzoefu usiopungua angalau miaka kumi katika ufundishaji au uongozi wa elimu; na

(d) mwenye kuheshimika katika jamii;

Kazi za Mkaguzi Mkuu wa Elimu.

14. Mkaguzi Mkuu wa Elimu atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Ofisi na atakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia shughuli za Ofisi kwa ufanisi;

(b) kusimamia upatikanaji wa mafanikio ya kiwango cha juu na ubora wa elimu katika skuli na kuhakikisha kuwa zinafuata masharti ya Sheria hii;

(c) kuwasilisha kwenye Bodi waraka wowote unaopendekezwa unaolenga kuimarisha mfumo wa ukaguzi kwa ajili ya kutolewa maamuzi;

(d) kupendekeza hatua za kinidhamu za kuchukuliwa dhidi ya mwalimu au mwalimu mkuu kwa mamlaka husika kwa kuzingatia ripoti ya ukaguzi;

(e) kukusanya, kuchambua na kutoa taarifa kwa Bodi za yaliyobainika katika ripoti ya ukaguzi ya robo mwaka na mapendekezo yake;

(f) kupendekeza maeneo ya kufanya utafiti kwa kuzingatia mambo yaliyobainika katika ripoti za ukaguzi wa elimu;

(g) kuunganisha pamoja Idara za Serikali, wadau wengine na washirika wa maendeleo katika ukaguzi wa elimu;

(h) kupendekeza uwajiri wa wafanyakazi wa Ofisi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma;

(i) kutayarisha ripoti za ukaguzi za robo mwaka, na za mwaka, mpango kazi na bajeti na kuziwasilisha kwenye vikao vya Bodi;

(j) kufuatilia ufanisi wa mafunzo ya uwalimu na kushauri vipaumbele na mahitaji kuhusiana na mafunzo ya walimu;

(k) kupima utendaji wa msimamizi wa skuli; na

(l) kufanya kazi nyengine yoyote inayohusiana na elimu kama itakavyoelekezwa na Waziri.

Uwezo wa Mkaguzi Mkuu wa Elimu.

15.-(1) Mkaguzi Mkuu wa Elimu atakuwa na uwezo wa :

(a) Kuelekeza skuli ikaguliwe na mkaguzi mmoja au zaidi kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba skuli inafuata masharti ya Sheria hii na kuhakikisha kwamba skuli hiyo imekaguliwa ipasavyo;

(b) Kuingia katika eneo lolote la skuli katika kutekeleza majukumu yake;

(c) Kumuagiza mwalimu mkuu, msimamizi au mwalimu, kuwasilisha waraka wowote, kutoa maelezo katika nakala ngumu au nakala laini zinazohusiana na utawala, uendeshaji, ufundishaji au kujifunza;

(d) Kuchukua nakala ya waraka au kuelekeza ipelekwe kwenye Ofisi ya Mkaguzi ya Mkoa au Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi; na

(e) Kupendekeza kwa mamlaka husika kuhusiana na utowaji wa zawadi au adhabu dhidi ya mwalimu au mwalimu mkuu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake, Sheria ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na kanuni zake na sheria nyengine zinazohusika za kazi.

(2) Mkaguzi Mkuu wa Elimu anaweza kukasimu madaraka yake kwa wakaguzi wa mikoa kwa kutumia uwezo wake uliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) (a) cha kifungu hiki kwa utekelezaji bora wa Sheria hii.

Uteuzi wa Naibu Mkaguzi Mkuu wa Elimu.

16.-(1) Rais anaweza kumteuwa mtu mwenye sifa kuwa Naibu Mkaguzi Mkuu wa Elimu kwa madhumuni ya kutekeleza masharti ya Sheria hii.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Naibu Mkaguzi Mkuu wa Elimu ikiwa :

(a) ni Mzanzibari;

(b) mwenye angalau Shahada ya Kwanza katika fani ya elimu au inayolingana na hiyo kutoka katika Chuo Kikuu kinachotambulika;

(c) mwenye uzoefu usiopungua angalau miaka kumi katika ufundishaji au Uongozi wa Elimu; na

(d) mwenye kuheshimika katika jamii.

Kazi za Naibu Mkaguzi Mkuu.

17. Naibu Mkaguzi Mkuu wa Elimu atakuwa Msaidizi Mkuu wa Mkaguzi Mkuu, atafanya kazi zote na atakuwa na uwezo wote wa Mkaguzi Mkuu, na atafanya kazi nyengine yoyote atakayopewa na Mkaguzi Mkuu kila baada ya muda.

Kuanzishwa kwa Ofisi za Ukaguzi za Mikoa.

18. Kutaanzishwa Ofisi za Ukaguzi za Mikoa katika mikoa yote ya Zanzibar.

Uteuzi wa Mkuu wa Ukaguzi wa Mkoa.

19.-(1) Kutakuwa na Mkuu wa Ukaguzi wa Mkoa ambae atateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Ukaguzi wa Mkoa ikiwa :

(a) ni Mzanzibari;

(b) mwenye angalau shahada ya kwanza katika fani ya elimu au inayolingana na hiyo kutoka katika Chuo Kikuu kinachotambulika;

(c) mwenye uzoefu usiopungua miaka kumi katika kazi ya ualimu na angalau miaka mitano katika Ukaguzi wa Elimu; na

(d) mwenye kuheshimika katika jamii.

Kazi za Mkuu wa Ukaguzi wa Mkoa.

20. Kazi za Mkuu wa Ukaguzi wa Mkoa zitakuwa ni:

(a) kutayarisha mpango wa ukaguzi wa skuli katika mkoa;

(b) kupendekeza mpango wa mafunzo ili kuimarisha ubora wa ufundishaji katika mkoa;

(c) kuwasilisha nakala za ripoti ya ukaguzi ya mkoa wake katika Ofisi na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya;

(d) kuwasilisha ripoti za ukaguzi kwa mamlaka husika kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 8 cha sheria hii;

(e) kufanya utafiti kwa mambo yanayohusiana na ukaguzi wa elimu;

(f) kuchambua na kuwasilisha kwa Mkaguzi Mkuu wa Elimu taarifa za yaliyobainika katika ripoti ya ukaguzi ya robo mwaka; na

(g) kufanya kazi nyengine yoyote atakayoagizwa na Mkaguzi Mkuu wa Elimu kila baada ya muda.

Uteuzi wa Mkaguzi wa Elimu.

21.-(1) Kutakuwa na Mkaguzi wa Elimu ambae atateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkaguzi wa Elimu ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) mwenye angalau stashahada katika fani ya elimu kutoka katika Chuo Kikuu au taasisi ya mafunzo ya elimu inayotambuliwa;

(c) mwenye uzoefu usiopungua angalau miaka kumi katika kazi ya ufundishaji; na

(d) mwenye kuheshimika katika jamii.

(3) Waziri anaweza, kwa kushauriana na Bodi, kumsimamisha au kufuta uteuzi wowote chini ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki ikiwa kufanya hivyo kutakuwa ni kwa maslahi ya umma.

Kazi za Mkaguzi wa Elimu.

22. Kazi za Mkaguzi wa Elimu zitakuwa ni:

(a) Kufanya ukaguzi kwa skuli yoyote na mwalimu yeyote kwa lengo la kutoa msaada wa kitaaluma kwa kuzingatia viwango vya uongozi wa skuli na utawala, ufundishaji na ujifunzaji, msaada kwa wanafunzi na matokeo ya kujifunza kwa mujibu wa Mfumo wa Ukaguzi uliowekwa na Ofisi;

(b) Kusimamia utekelezaji wa mtaala kwa utaratibu unaotumika katika skuli;

(c) Kuandika na kutoa mrejesho wa ukaguzi kwa skuli na mwalimu mmoja mmoja na kuwasilisha nakala ya ripoti ya ukaguzi kwa Mkuu wa Ukaguzi wa Mkoa;

(d) Kufanya ukaguzi kwa taasisi yoyote ya elimu kwa lengo la kuhakiki au kuthibitisha usajili wake; na

(e) Kufanya kazi nyengine yoyote atakayopewa na Mkuu wa Ukaguzi wa Mkoa kila baada ya muda.

Uwezo wa Mkaguzi wa Elimu.

23. Mkaguzi wa Elimu atakuwa na mamlaka yafuatayo:

(a) kuingia katika eneo lolote la skuli katika kutekeleza majukumu yake;

(b) kumuagiza Mwalimu Mkuu, Msimamizi au Mwalimu kuwasilisha waraka wowote, kutoa maelezo katika nakala ngumu au laini zinazohusiana na utawala, uendeshaji, ufundishaji au ujifunzaji.

(c) kuchukua nakala ya waraka au kuagiza ipelekwe kwa Ofisi ya ukaguzi ya Mkoa kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi;

Kutoa taarifa kwa asiyehusika.

24.-(1) Ni marufuku kwa Mkaguzi kutangaza au kutoa taarifa za mwalimu, wafanyakazi au skuli kwa mtu yeyote au taarifa zinazohusiana na ukaguzi ambazo anazifahamu katika kutekeleza majukumu yake isipokuwa kwa mamlaka husika.

(2) Mkaguzi yeyote atakaekwenda kinyume na kifungu hiki ametenda kosa na atakapopatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni tano za kitanzania au kifungo cha muda usiozidi mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo.

Wajibu wa Mwalimu Mkuu au Meneja na Mwalimu.

25.-(1) Mwalimu Mkuu au Meneja atakuwa na wajibu wa kufanya ukaguzi wa ndani, kufundisha na kutekeleza majukumu yote ya uongozi kama ilivyoainishwa katika miongozo ya Wizara.

(2) Mwalimu Mkuu au Meneja na Mwalimu watakuwa na wajibu wa kuwa tayari kukaguliwa wakati wowote.

(3) Mwalimu Mkuu au Meneja na Mwalimu watalazimika kuufanyia kazi ushauri na maelekezo yaliyotokana na ripoti za ukaguzi.

(4) Mwalimu atakuwa na wajibu wa kufanya maandalizi ya kufundisha kwa kuwa na azimio la kazi, andalio la somo, kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi, kumbukumbu za kazi za kila siku na vifaa vyenginevyo vinavyohusika katika ufundishaji.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA FEDHA

Fedha na rasilimali.

26. Fedha na rasilimali za Ofisi zitajumuisha:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar; na

(b) fedha nyengine yoyote Ofisi itakayoweza kupewa au kuipata kihalali.

Matumizi ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

27. Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine zinazohusiana na fedha za Umma zitatumika katika miamala yote ya kifedha na masuala yanayohusiana na Ofisi.

Hesabu na ukaguzi.

28.-(1) Hesabu za Ofisi zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu au mkaguzi mwengine aliyeidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu.

(2) Mkaguzi Mkuu wa Elimu atalazimika kuwasilisha hesabu zilizokaguliwa ikijumuisha taarifa za matumizi ya fedha za Ofisi yake kwa Bodi ya Ushauri ndani ya miezi miwili baada ya kufunga hesabu za mwaka wa fedha.

Bajeti.

29. Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu itaandaa Bajeti ya mwaka kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha.

SEHEMU YA NNE
MAKOSA NA ADHABU

Kutoa taarifa za uongo au za kupotosha.

30. Mtu yeyote ambaye atatoa taarifa za uongo au za kupotosha atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi za kitanzania Laki Tano na isiyozidi shilingi Milioni Tano au kifungo cha muda usiozidi mwaka mmoja, au vyote viwili faini na kifungo.

Kumzuwia Mkaguzi wa Elimu.

31. Mtu yeyote ambaye kwa makusudi atakataa, atamchelewesha, atamkwamisha au atamzuwia Mkaguzi yeyote wa Elimu kutekeleza majukumu yake, atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Tano na isiyozidi Shilingi Milioni Tano au kifungo cha muda usiozidi mwaka mmoja, au vyote viwili faini na kifungo.

Kushindwa kutekeleza majukumu.

32.-(1) Pale ambapo, kwa madhumuni ya ukaguzi, mwalimu atakaebainika kushindwa kutekeleza majukumu yake kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 25 cha Sheria hii, msimamizi wa skuli baada ya kupokea taarifa ya ukaguzi atalazimika, ndani ya miezi mitatu, kuchukua hatua za kinidhamu, kwa mujibu wa Sheria hii, Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria nyengine zinazohusika za kazi.

(2) Msimamizi yeyote atakaekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Mbili na isiyozidi Laki Tano.

(3) Pale ambapo, kwa madhumuni ya ukaguzi, msimamizi atabainika kushindwa kufuata viwango vya taaluma, maadili ya kazi, kanuni za ukaguzi, miongozo ya utendaji kazi au miongozo mengine inayohusika, katika utekelezaji wa majukumu yake, mamlaka husika ya skuli baada ya kupokea taarifa ya ukaguzi analazimika, ndani ya miezi mitatu, kuchukua hatua, kwa mujibu wa Sheria hii, Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria nyengine zinazohusika za kazi.

(4) Mamlaka husika ya skuli ambayo itakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana

na hatia atalazimika kulipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Mbili na isiyozidi Laki Tano.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI MENGINEYO

Kufungwa kwa Skuli kwa maslahi ya Umma.

33. Iwapo Waziri, baada ya kupokea ripoti ya ukaguzi, ataridhika kwamba kuachiwa skuli iendelee kufanya kazi si kwa maslahi ya umma, anaweza, kwa kupitia tangazo katika Gazeti Rasmi, kuamrisha kufungwa skuli au sehemu ya skuli, kutegemea na hali itakavyokuwa, kwa muda, au moja kwa moja na kufuta usajili wake na anaweza kuzifunguwa tena skuli hizo itakapoonekana inafaa.

Uwezo wa Waziri kutunga kanuni.

34.-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza, kutunga kanuni mahsusi kuhusiana na:

(a) majukumu na wajibu wa waajiri, wasimamizi na walimu kuhusiana na ukaguzi wa elimu; na

(b) hatua za kuchukuliwa kwa mamlaka husika baada ya kupokea ripoti ya ukaguzi.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2) cha kifungu hiki, Bodi inaweza kuweka miongozo ikijumuisha mambo yafuatayo:

(a) miongozo ya kazi juu ya utaratibu wa ukaguzi wa elimu; na

(b) utekelezaji wa mfumo wa ukaguzi wa elimu.

Kufuta na kubakiza.

35.-(1) Sehemu ya VI ya Sheria ya Elimu Nam. 6 ya mwaka 1982 inafutwa.

(2) Kitu chochote kilichofanywa chini ya sehemu ya VI iliyofutwa itachukuliwa kwamba yamefanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

JADWELI

Utaratibu wa Bodi
[Chini ya kifungu cha 10 (4)]

Muda wa Bodi.

1.-(1) Mwenyekiti wa Bodi atatumikia wadhifa wake kwa muda wa miaka minne kuanzia tarehe ya uteuzi na anaweza kuteuliwa tena.

(2) Isipokuwa wajumbe walioteuliwa kwa nafasi zao ki-Ofisi, Wajumbe wengine wa Bodi, isipokuwa pale ambapo mjumbe uteuzi wake umekoma au umesitishwa kwa njia nyengine yoyote, watatumikia wadhifa wao kwa muda wa miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena.

Makamu Mwenyekiti.

2. Bodi itamchagua mmoja miongoni mwa wajumbe wake kuwa Makamu Mwenyekiti.

Vikao vya Bodi.

3.-(1) Bodi itafanya vikao vyake vya kawaida katika kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana wakati wowote itakapohitajika kufanya hivyo katika kutekeleza majukumu yake.

(2) Taarifa za vikao zilizoambatana na nyaraka za mkutano zitatolewa kwa wajumbe wa Bodi si chini ya siku saba kabla ya kikao.

(3) Mwenyekiti ataendesha vikao vyote vya Bodi na akiwa mwenyekiti hayupo Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao, na iwapo wote hawapo mwenyekiti na Makamu mwenyekiti, wajumbe waliopo watamchagua mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Kusita kuwa Mjumbe.

4.-(1) Mjumbe wa Bodi atasita kuwa mjumbe iwapo:

(a) Atafariki ;

(b) Atashindwa kutekeleza kazi zake za ofisi;

(c) amekiuka maadili au utovu wa nidhamu;

(d) ametiwa hatiani kwa kosa la jinai ikijumuisha udanganyifu, kukosa uaminifu au ukosefu wa maadili;

(e) ameshindwa kuweka bayana kuwa ana maslahi kuhusiana na suala lililojadiliwa katika kikao;

(f) kutokuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila ya ruhusa ya mwenyekiti; au

(g) amejiuzulu kwa kutoa indhari kwa mamlaka iliyomteuwa na kutoa sababu ya kujiuzulu huko.

(2) Iwapo mjumbe wa Bodi, isipokuwa kwa mjumbe kwa nafasi yake, atasita kuwa mjumbe kwa sababu yoyote iliyotolewa chini ya

kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kabla ya kumaliza muda wake wa kutumikia wadhifa wake, mamlaka ya uteuzi itamteuwa mtu mwengine kushika nafasi yake, na mtu huyo aliyeteuliwa atatumikia Ofisi kwa muda uliobaki kwa mtangulizi wake.

Akidi ya kikao.

5. Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wataunda Akidi ya kikao cha Bodi.

Maamuzi ya Bodi.

6.-(1) Maamuzi ya Bodi yatafikiwa kwa makubaliano ya wajumbe na itakapotokoa kutokukubaliana maamuzi yatafikiwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria na kupiga kura, iwapo ikitokea kura za wajumbe kuwa sawa, mwenyekiti au mtu anaeongoza kikao atakuwa na kura ya maamuzi.

(2) Bila ya kujali aya ndogo ya (1) ya aya hii, maamuzi yanaweza kufanywa na Bodi kwa kusambaza nyaraka kwa wajumbe ambapo kila mjumbe ataeleza mtazamo wake kwa maandishi, isipokuwa kwamba, mjumbe yeyote anaweza kuagiza maamuzi hayo yapelekwe kwa ajili ya majadiliano katika vikao vinavyofuata.

(3) Azimio la maandishi linalotokana na nyaraka zilizosambazwa kwa wajumbe walioko Zanzibar wasiopungua watano itachukuliwa kwamba ni maamuzi kamili ya kikao.

Kumualika mtu.

7. Bodi inaweza kumualika mtu au watu wowote katika kikao chake chochote lakini mtu aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura katika kikao chochote kwa jambo lolote ambalo Bodi inalitolea maamuzi.

Katibu wa Bodi.

8.-(1) Bodi itamteua Afisa Sheria mwenye uzowefu wa Ofisi kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Katibu hatokuwa na haki ya kupiga kura katika azimio lolote.

(3) Katibu wa Bodi atachukuwa na kuhifadhi kumbukumbu za vikao vya Bodi.

(4) Kumbukumbu za vikao vya Bodi zitasomwa na kuthibitishwa na Bodi katika kikao chake kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu wa Bodi.

Utaratibu wa vikao.

9. Kwa kuzingatia masharti ya Jadweli hili, Bodi itakuwa na uwezo wa kujipangia utaratibu wake wa uendeshaji wa vikao.

Mgongano wa maslahi ya mjumbe.

10. Mjumbe ambaye anamaslahi ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja katika jambo linalotaka kujadiliwa katika kikao cha Bodi atapaswa kueleza maslahi aliyonayo kwa Bodi na hatoshiriki katika maazimio yanayohusiana na suala linalotaka kujadiliwa.

Kuanzishwa kwa kamati na vitengo.

11.-(1) Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kutekeleza kazi zake, kuanzisha kamati au vitengo kufanya kazi mahsusi kama vitakavyopewa na Bodi.

(2) Utaratibu, makubaliano na mambo mengine yanayohusiana na kamati au vitengo hivyo vitakavyoanzishwa utakuwa kama utakavyoelezwa na Bodi.

12. Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi, kamati na vitengo watapaswa kulipwa posho na ada katika kiwango ambacho kitaamuliwa na kuthibitishwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Posho za Wajumbe.

MADHUMINI NA SABABU

Madhumuni makuu ya mswada huu ni kuanzisha wakala wa Serikali unaojulikana kama Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu utakaosimamia na kufuatilia utoaji wa elimu bora Zanzibar katika skuli zote zinazotoa elimu ya maandalizi, msingi na sekondari, taasisi yoyote inayotoa mafunzo ya ualimu, elimu ya watu wazima na vituo vya elimu mbadala na taasisi za elimu zilizosajiliwa zilizo nje ya mfumo rasmi wa elimu.

Mswada unaopendekezwa umekusudia kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa ndani ya Zanzibar inatolewa kwa mujibu wa Sera, Sheria na miongozo mbali mbali ya Serikali, na kuhakikisha kuwa viwango vya elimu na uthibiti ubora vinafuatwa katika ngazi zote za skuli na kwenda sambamba na Miongozo ya Wizara.

Mswada umegawika katika Sehemu Tano:

Sehemu ya kwanza inaelezea masharti ya awali ikijumuisha jina fupi na kuanza kutumika, matumizi na tafsiri ya maneno yaliyotumika katika mswada huu.

Sehemu ya pili inaelezea masharti yanayohusiana na uanzishwaji wa Ofisi, muhuri na nembo ya Ofisi, malengo ya Ofisi, mfumo wa ukaguzi wa elimu, uwasilishaji wa ripoti za ukaguzi, kazi za Ofisi, kuanzishwa kwa Bodi ya Ushauri, sifa za mwenyekiti, kazi za Bodi ya Ushauri, uteuzi wa mkaguzi mkuu wa elimu, kazi za mkaguzi mkuu wa elimu, uwezo wa mkaguzi mkuu wa elimu, nteuzi wa naibu mkaguzi mkuu wa elimu, kazi za naibu mkaguzi mkuu, kuanzishwa kwa Ofisi za mkaguzi za mikoa, uteuzi wa mkuu wa ukaguzi wa mkoa, kazi za mkuu wa ukaguzi wa mkoa, uteuzi wa mkaguzi wa elimu, kazi za mkaguzi wa elimu, uwezo wa mkaguzi wa elimu, kutoa taarifa kwa asiyehusika na wajibu wa mwalimu mkuu au meneja na mwalimu.

Sehemu ya tatu inaelezea mambo yanayohusiana na masharti ya fedha ikijumuisha Fedha na raislimali, matumizi ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, hesabu na ukaguzi na bajeti.

Sehemu ya nne inahusiana na makosa na adhabu, sehemu hii imeweka vifungu vya Kutoa taarifa za uongo au za kupotosha, kumzuwia mkaguzi wa elimu na kushindwa kutekeleza majukumu.

Sehemu ya tano inahusiana na masharti ya jumla yanayojumuisha kufungwa kwa Skuli kwa maslahi ya umma, uwezo wa Waziri kutunga kanuni na kufuta na kubakiza.

Mswada pia unajumuisha jadweli linalohusu utaratibu wa Bodi ya Ushauri.

(RIZIKI PEMBE JUMA)
WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI
ZANZIBAR.

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR - 2018